

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA TISA

19 APRILI, 2017



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA TISA– TAREHE 19 APRILI, 2017

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

70. MHESHIMIWA FREDY ATUPELE MWAKIBETE (BUSOKELO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itayakubali maombi ya Wananchi wa Halmashauri ya Busokelo ya kuifanya Halmashauri hiyo iwe Wilaya.

71. MHESHIMIWA JOEL MWAKA MAKANYAGA (CHILONWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia maji Wananchi wa Vijiji vya Jimbo la Chilonwa.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

72. MHESHIMIWA SAVERINA SILVANUS MWIJAGE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:- Nyumba za Shirika la Nyumba Nchini (NHC) ni za muda mrefu na zimekuwa chakavu sana na nyingine zimeanza kubomoka:-

- (a) Je, ni lini Serikali itafanya operesheni kubaini uharibifu ulioko kwenye nyumba hizo;
- (b) Je, ni lini Serikali itatenga bajeti kwa ajili ya kukarabati au kujenga upya nyumba hizo.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

73. MHESHIMIWA CATHERINE VALENTINE MAGIGE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Waliokuwa wafanyakazi wa Hoteli ya Seventy Seven ya Arusha hawajalipwa mafao yao hadi sasa:-

Je, ni lini watalipwa mafao yao.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

74. MHESHIMIWA MOHAMED OMARY MCHENGERWA (RUJIFI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Matatizo ya mipaka kati ya wanakijiji na maeneo ya hifadhi husababisha migogoro kati ya wanakijiji na watumishi wa hifadhi:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kurejesha mahusiano kati ya watumishi wa hifadhi na wananchi.

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

75. MHESHIMIWA JOSEPH LEONARD HAULE (MIKUMI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Mradi wa Maji wa Madibira ulianzishwa mwaka 1975 na sasa miundombinu yake imechakaa sana na banio (*intake*) lake limekuwa dogo sana wakati idadi ya watu imeongezeka sana:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kukarabati miundombinu hiyo ili kuwaokoa Wananchi wa Mikumi na taabu ya maji.

**76. MHESHIMIWA PAULINE PHILIPO GEKUL
(BABATI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:-

Je, ni lini Serikali itafanya tathmini ya miradi ya maji ya visima 10 katika Vijiji inayofadhiliwa na Benki ya Dunia.

**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA
AFRIKA MASHARIKI:**

**77. MHESHIMIWA BALOZI DKT. DIODORUS
BUBERWA KAMALA (NKENGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:- Jumuiya ya Ulaya inatekeleza Mkakati wa Agenda ya Mabadiliko:-

Je, Tanzania imejipangaje kukabiliana na changamoto zinazotokana na Agenda hiyo ya Mabadiliko ya Jumuiya ya Ulaya.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

**78. MHESHIMIWA SUBIRA KHAMIS MGALU
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya kutoka Kisarawe – Manerumango km 64 itajengwa kwa lami na kukamilika kama ilivyoahidiwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015.

**79. MHESHIMIWA DKT. RAPHAEL MASUNGA
CHEGENI (BUSEGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Kumekuwa na ahadi ya kujenga upya Gati la Nyamikoma – Busega ili kuboresha usafirishaji wa mizigo na mazao ya Samaki katika Ziwa Victoria:-

Je, ni lini utengenezaji huo utanza na kukamilika.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
19 APRILI, 2017**



**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**